



Maswali Na Majibu (Matibabu)

Q. Kuna dawa ya kutibu ugonjwa wa ukimwi?

Hapana, hakuna dawa ya kutibu ugonjwa wa ukimwi lakini kuna matibabu ya watu wanaoishi na virusi vya ukimwi ambazo huwasaidia kuishi na afya na pia kuishi maisha marefu.

Q. Matibabu ya ugonjwa wa ukimwi ni nini?

Matibabu ya kwanza ya ugonjwa wa ukimwi ulitengenezwa mwaka wa elfu moja mia tisa themanini na sita. Kuna matibabu aina mingi kama vile nevirapine ambayo ni rahisi na hutumiwa kuzuia mama kupitishia mwanaye virusi wakati ana mimba. Ile matibabu ambayo hutumiwa sana inaitwa HAART.

Q. Kwanini kuna matibabu aina mingi?

Virusi vya ukimwi hubadilika kila wakati kama ugonjwa zingine, kila wakati inabadilika basi matibabu inawacha kuwa na nguvu ama inachukuwa muda mrefu kufanya kazi pia virusi hivi hubadilika haraka na kwa wakati mfupi, kwasababu ya virusi kubadilika kila wakati matibabu huwacha kufanya kazi na hii ndio sababu kubwa kwanini kuna matibabu aina mingi ambayo yametengenezwa.

Q. Matibabu haya yanaweza kukuumiza?

Matibabu ya aina yote yana makosa saa zingine kama vile matibabu kukosa kufanya kazi.

Pia matibabu kufanya wagonjwa kuhisi vibaya kama vile kuhisi kutapika. Pia matibabu kuwa na wakati moja wa kumeza na pia kula lisho bora ili dawa iweze kufanya kazi.

Matibabu yanaweza kuwa na madhara saa zingine lakini matibabu haya husaidia watu wanaoishi na virusi vya ukimwi kuishi maisha marefu.

Q. Gharama inahusiana aje na matibabu?

Gharama inahusiano kubwa na matibabu, hapo awali matibabu yalikuwa ghali sana na watu tajiri pekee ndio waliweza kupata matibabu lakini kumekuwa na mabadiliko kutoka mwaka wa elfu mbili na moja kwani matibabu yamekuwa rahisi –dola mia mbili na themanini(280\$) kwa mwaka.